



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. EB.89/286/02.A/07

28/08/2023

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara anapenda kuwatangazia Wananchi wote kuwa kuna nafasi ya kazi ya Mkataba kama ifuatavyo:-

1. MSAIDIZI WA HESABU II: NAFASI (02)
2. SIFA ZA KUAJIRIWA- MSAIDIZI WA HESABU II.

Mwombaji anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

Awe muhitimu wa kidato cha Nne aliyehitimu mafunzo ya Astashahada (Cheti) cha ATEC level I au "Foundation level" cha masuala ya fedha kinachotolewa na NBAA au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

3. MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA HESABU II

- I. Kuandika na kutunza register zinazohusu shughuli za uhasibu
- II. Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya fedha
- III. Kutunza majalada yenye kumbukumbu za hesabu
- IV. Kupeleka barua /nyaraka za uhasibu Benki
- V. Kufanya usuluhisho wa masurufu, karadha, hesabu za kibenki na Amana

4. MSHAHARA – NGAZI YA MSHAHARA ITAKUWA NI TGS/B/1

5. MASHARTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI:-

- (i) Awe ni Raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 - 45
- (j) Awe Mtanzania Me/Ke mwenye akili timamu
- (k) Barua za mwombaji ziambatishwe pamoja na Vivuli (Photocopies) vya vyeti vya taaluma, ujuzi, kuzaliwa na picha mbili (2) (Passport size) za rangi za hivi karibuni, Nakala ya kitambulisho cha (NIDA) bila kusahau maelezo binafsi (CV) yanayojitosheleza yakionyesha anuani kamili za Wadhamini watatu (3). Namba ya simu ya Mwombaji ni muhimu na iandikwe katika barua ya maombi ya Kazi chini ya anuani yake.
- (l) Waombaji waliosomea nje ya nchi waambatishe uthibitisho wa Vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA).

- (m) Maombi yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili/Kiingereza.
- (n) Kwa waombaji ambao tayari wameisha ajiriwa/ walishawahi kufanya kazi Serikalini na kuacha kazi, wafanyakazi wanaotoka kuhama kada wanashauriwa kuzingatia utaratibu wa uhamisho au kurejea katika Utumishi wa Umma baada ya kuacha kazi kama ilivyoelekezwa katika Waraka Na. CCB.228/271/01 wa tarehe 07/08/2012.
- (o) Awe hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya Jinai.
- (p) Hati za matokeo ya kidato cha Nne na Sita (Statement of Results) hazitapokelewa.

6. MAOMBI YOTE YATUMWE KWA ANUANI IFUATAYO:-

**Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ngara,
S.L.P. 30,
NGARA.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **10/09/2023** saa **9:30** alasiri.


Emmanuel P. Kulwa
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI

Nakala:-

- Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,
S.L.P. 670,
DODOMA.
- Katibu Tawala (M),
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L.P. 299,
BUKOBA – KAGERA.
- Katibu Tawala (W),
Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,
S.L.P.20,
NGARA.
- Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mtaa,
MKOA WA KAGERA.
- Mbao zote za Matangazo,
Halmashauri ya Wilaya,
NGARA.

.L.P 30, Ngara, Simu:028 2226016, Nukushi:028 2226152, Barua pepe:ded@ngaradc.go.tz, Tovuti:
www.ngaradc.go.tz